

## **Uasilishaji wa Maneno ya Kigeni katika Lugha za Kiafrika: Mfano wa Kitharaka**

*Mwenda Mukuthuria<sup>1</sup>, Kimathi Mwembu<sup>2</sup> na Enock Matundura<sup>2</sup>*

<sup>1</sup>*Chuo Kikuu cha Maasai Mara*

<sup>2</sup>*Chuo Kikuu cha Chuka*

### **Ikisiri**

Kila lugha hukopa maneno ya kigeni na kisha kuyaasilisha ili yaafiki mfumo wa kifonolojia wa lugha pokezi. Kitharaka ni lugha iliyokopa maneno na kuyaasilisha kwa mujibu wa mfumo wa fonolojia yake. Makala haya yanaweka wazi mchango wa michakato ya kifonolojia katika kufanikisha uasilishaji wa maneno ya kigeni katika Kitharaka. Kitharaka ni lahaja ya lugha ya Kimeru inayozungumzwa nchini Kenya. Uasilishaji wa maneno ya kigeni kutoka lugha mbili changishi (ambazo ni Kiswahili na Kiingereza) hadi Kitharaka umeangaziwa. Jumla ya michakato minane ya kifonolojia imeshughulikiwa kama vile uchopekaji wa sauti, kuimarike kwa fonimu, kudhoofika kwa fonimu, ukaakaishaji, ung'ong'oishaji, usilimisho, usilabishwaji na uwiano wa irabu. Hatimaye, makala haya yamependekeza uchunguzi zaidi ufanywe ili kuweka wazi jinsi michakato ya kifonolojia katika Kitharaka inavyokamilishana. Vilevile, makala haya yamependekeza uasilishaji wa maneno ya kigeni katika lugha nydingine za Kiafrika uchunguzwe ili kubainisha jinsi lugha hizi zinavyokamilishana na kufaana kukabiliana na changamoto za mawasiliano katika kipindi hiki cha utandawazi.

**Maneno Muhimu:** *Uasilishaji, Fonolojia, Kitharaka, Maneno ya Kigeni, Lugha za Kiafrika*

### **Utangulizi**

Kuwepo kwa maneno mageni katika lugha za ulimwengu ni suala lisiloweza kuepukwa ama kupuuza. Hii ni kwa sababu wazungumzaji wa lugha mbalimbali wanapotangamana katika shughuli tofautitofauti, lugha zao huathiriana. Mukuthuria (2008) anasema kuwa hamna lugha yoyote ambayo haijaathiriwa na kwamba nydingi ya athari zinazoingilia lugha huwa na manufaa makubwa ya kuiwezesha lugha husika kujitosheleza kimawasiliano. Athari mojawapo ya mtagusano wa lugha mbili au zaidi ni ukopaji wa msamati (Anderson, 1973; Appel & Muysken 1987; Crystal 1987). Kuingizwa kwa maneno mageni katika lugha hutokana na haja ya lugha ya kutaka kufanikisha mawasiliano. Lugha mbili au zaidi zikitagusana, ile iliyosheheni utamaduni ulioendelea zaidi kiteknolojia ndiyo huchangia maneno mengi kwenye lugha ambayo utamaduni wake haujaendelea sana kiteknolojia (Mwihaki, 1998). Kwa mfano, Kiingereza ndiyo lugha changishi kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na

lugha za Kiafrika. Katika mtazamo sawa na huu, Kiswahili, kikilinganishwa na lugha nyingine za Kiafrika, huwa lugha changizi kwa kiasi kikubwa kwa sababu Waswahili walitangamana na Waarabu na wageni wengineo kwa karne nyingi, hali ambayo ilikifanya Kiswahili kukopa msamiati wa kiteknolojia kutoka lugha mbalimbali, Kiarabu kikiwemo (Zawawi, 1974; Mwita, 2009). Ni kutokana na hali hii ambapo mada ya makala haya imejikita katika kuchunguza dhima ya michakato ya kifonolojia katika kufanikisha uasilishaji wa maneno mageni yanayoingizwa kwenye lugha pokezi. Ili kufafanua mchango huu, makala haya yameifafanua michakato ya kifonolojia inayofanikisha uasilishaji wa maneno mageni kwa mujibu wa fonolojia ya Kitharaka.

Kitharaka kinasheheni maneno mengi ambayo ni mageni; kwa kiasi kikubwa kutoka kwa lugha changishi mbili kuu, ambazo ni: Kiingereza na Kiswahili. Kwa hiyo, katika makala haya, maneno mageni yaliyohusishwa yametokana na lugha hizi mbili. Kwa mfano, maneno yafuatayo ni mageni na yameasilishwa kwa mujibu wa fonolojia ya Kitharaka.

<b>Kiswahili</b>	<b>Kitharaka</b>
[pesa] pesa	→ [mbeca] mbeca
<b>Kiingereza</b> [hospitl] hospital	<b>Kitharaka</b> → [cibitare] cibitarī

Kwa kuzingatia mifano iliyoko hapo juu, inatokea kwamba maneno mageni katika lahaja ya Kitharaka hupitia michakato fulani ya kifonolojia ili yaafikiane na fonolojia ya lugha pokezi.

### Asili ya Kitharaka

Lahaja ya Kitharaka ni moja kati ya lahaja saba za Kimeru. Lahaja nyingine ni Kitigania, Kiigembe, Kiimenti, Kichuka, Kimuthambi na Kimwimbi. Lahaja hizi zote awali zilijumlishwa katika wilaya ya Meru Kuu ya zamani. Hivi leo, Kitharaka ni lahaja inayozungumzwa katika kaunti ya Tharaka-Nithi na Kitui, nchini Kenya. Mgawo huu mpya wa maeneo unatokana na ugatuza wa mamlaka ulioletwa na katiba mpya iliyopitishwa 2010.

### Dhana ya Uasilishaji

Msamiati mgeni hubidi kuasilishwa angalau kifonolojia ili uafikiane na mfumo wa kifonolojia wa lugha pokezi (Anderson, 1973; Hudson, 1980). Hii ni kwa sababu kila lugha hutofautiana na nyingine kwa kiwango fulani (Katamba, 1989). Hivi ni kusema kwamba hapana budi kuwepo kwa mabadiliko ya kifonolojia lugha moja inapopata msamiati mgeni. Mabadiliko ya maneno magenihutokea katika viwango viingine vytaa kama vile kiwango cha fonetiki, mofolojia, sintaksia na hata leksia (Mosha, 1970). Jambo hili linapotoka lugha pokezi huwa na mbinu mahususi za kuingiza vipashio vinavyokopwa katika mfumo wake katika viwango vyote tulivyovitaja hapo juu. Kati ya viwango vyote hivicha kimsingi zaidi katika

uasilishaji wa maneno mageni katika lugha ni kile cha kifonolojia (Kadurenge, 2000). Kwa mujibu wa Hearth (1994), mbinu za uasilishaji huhusisha michakato ya ndani kwa ndani ya lugha pokezi, ambayo aghalabu huwa hajadhihirika kwa urahisi.

Dhana ya uasilishaji hujidhihirisha kwa njia mbili: Kwanza, ile inayochukuliwa kama mchakato wa lugha fulani kupata wazungumzaji asilia (Gillian & Suzanne, 1972). Wanaismu hawa wanaeleza kuwa aina hii ya uasilishaji hulazimika kutokea wakati lugha ya pili ya wazazi hugeuka na kuwa lugha asilia ya wazawa wao. Aina ya pili ya uasilishaji huhusu mabadiliko yanayolazimika kutokea kwenye maneno mageni yanapoingia katika lugha pokezi. Aina hii ya pili ndiyo tuliyochunguza katika makala haya.

Uasilishaji umejelezwa kama hali ya ubadili inayohusu utohozi wa maumbo kifonolojia (Mwiaki, 1998). Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, uasilishaji wa maneno mageni hauwezi kutenganishwa na utohozi. Maneno mageni yanayoasilishwa lazima yapitie katika hatua ya utohozi kifonolojia. Katika mwelekeo sawa na huu, tunapata Kamusi Sanifu ya Lugha na Isimu (1990) ikifafanua utohozi kama utaratibu wa kubadili maumbo ya maneno yaliyo mageni katika lugha ili yakubaliane na mfumo wa lugha pokezi-hasa katika kiwango cha kifonolojia. Mwita (2009) anasema kuwa uasilishaji na utohozi ni dhana zinazotumika kwa maana sawa. Kulingana na msomi huyu, uasilishaji ni hatua ya kidharura inayochukuliwa na lugha pokezi ili kutatua tatizo la kuwepo muundo mpya wa silabi unaosababishwa na maneno mageni. Katika hali hii muundo mpya wa silabi huenda kinyume na mfumo wa fonolojia wa lugha pokezi. Buliba (2001) anasema kwamba usilabishaji wa maneno mageni na ubadilishanaji wa vipandesauti vya lugha changishi na vya lugha pokezi ni baadhi ya mambo yanayopaswa kuchunguzwa yakihuhsisha na uasilishaji.

### **Michakato ya Kifonolojia inayofanikisha Uasilishaji wa Maneno Mageni**

Uasilishaji wa maneno mageni huongozwa na sheria mahususi ambazo huibuka kutokana na michakato ya kifonolojia inayoathiri fonimu na silabi katika neno. Akizungumzia suala hili, Buliba (2001) anasema kwamba kuna taratibu na kanuni au sheria kadha za kifonolojia ambazo huihusisha na, au kuiathiri silabi. Katika mwelekeo sawa na huu, watafiti wangependa kuchunguza baadhi ya michakato ya kifonolojia, na kisha kubaini jinsi inavyoathiri na huku ikifanikisha uasilishaji wa maneno mageni.

### **Uchopekaji wa Sauti**

Uchopekaji wa sauti husimamia kaida ya kuingiza sauti katika umbo asilia. Mchakato huu hutokea wakati wa uundai wa maneno, uambishaji wa maneno na uasilishaji wa maneno mageni (Mwiaki, 1998). Uchopekaji wa sauti ni utaratibu wa kifonolojia unaotumika kudhibiti muundo unaopendelewa wa maneno; ambao unaweza kutekelezwa kwa kuingizwa kwa sauti pale ambapo konsonanti au irabu mbili zinafuatana. Katika Kitharaka, uchopekaji wa sauti hupatikana katika maneno

mageni yanayoasilishwa kutoka Kiswahili na vilevile Kiingereza, kiasi kwamba, ama irabu au konsonanti inaweza kuchopekwa. Sauti inaweza kuchopekwa katika mazingira matatu tofauti ya neno; yaani mwanzoni, katikati na mwishoni mwa neno. Kuna mifano kadhaa ya maneno mageni ambayo yanadhihirisha uchopekaji sauti katika mazingira tofauti ya neno. Tutaanza na maneno ambayo kwayo uchopekaji wa sauti hutokea mwanzoni mwa neno.

Kiswahili	Kitharaka	Othografia
[rinda] ø→e/...#	→	[erinda] rinda
[ʃembə] ø→e/...# ʃ→c	→	[ecembə] jembe
[ubaɔ] ø→r/...# u→o ɔ→o	→	[robao] ubao
[ɛmbə] ø→j/...#	→	[jembe] embe

Katika mfano wa kwanza na wa pili, neno [rinda] na [ʃembə] yamechopekwa irabu /e/ ili kupata neno [erinda] ‘rinda’ na [ecembə] ‘cembe’ mtawalia. Uchopekaji katika maneno haya huyawezesha maneno husika kuingizwa katika ngeli ya kimofolojia inayofaa katika muktadha huu kulingana na mfumo wa mofonolojia wa Kitharaka. Katika hali hii, sauti /e/ inawakilisha kiambishi cha ngeli ya **î-ma** katika hali ya umoja na wingi. Katika mfano wa tatu na wa nne, konsonanti /r/ na /j/ zimechopekwa mwanzoni mwa maneno husika ili kufanikisha muundo bia wa silabi (KI). Kanuni ya jumla inayotawala aina hii ya uchopekaji ni: Ø→I(K)/...#. Vilevile, kuna uchopekaji wa sauti katikati mwa neno. Hali hii inadhihirika katika mifano ifuatayo:

Kiingereza	Kitharaka	Othografia
[breɪk] b→mb ø→u/K...K	→	[mbureki] brake
eɪ→e ø→i		
[klʌb] ø→e/K...K l→r ʌ→e ø→u/#...	→	[kerebu] club

Kiswahili	Kitharaka	Othografia
[mʃipi]	→	[mocibi] mshipi
ø→ø/K...K		
ʃ→c		
p→b		
i→i		
 [mkebe]	→	 [mokebe] mkebe
ø→ø/K__K		
ε→ε		

Uchopekaji wa irabu katika mazingira ya katikati mwa maneno yaliyoasilishwa katika Kitharaka umetokana na haja ya kuvunja mfuatano wa konsonanti mbili au zaidi. Hali hii hulazimika kutokea ili kudumisha ule muundo wa kimsingi wa silabi wa Konsonanti na Irabu (KI) ambao unapendelewa sana na lugha ya Kitharaka. Si kila siku ambapo maneno mageni kutoka Kiswahili yanayoingia katika Kitharaka huchopekwa irabu katikati mwa neno. Kuchopekwa irabu katika mazingira ya katikati mwa neno hutokea wakati neno linaloasilishwa limeundwa kwa silabi funge ya king'ong'o /m/ ikifuatiwa na silabi inayoanza na konsonanti. Kwa mfano, neno [mkebe] linachopekwa irabu /o/ ili kuvunja mfuatano wa konsonanti mbili /m,k/. Kimsingi, Kiswahili pia hupendelea silabi ya muundo wa (KI) kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu. Tofauti ni kuwa Kiswahili kinaaminika kupoteza muundo wa silabi wazi katika baadhi ya maneno yake (Mukuthuria, 2004). Pia, irabu huchopekwa mwishoni mwa neno na hali hii hutokea ikiwa silabi ya mwisho ya neno ni funge. Hii ni kwa sababu maneno yote yanayoasilishwa katika Kitharaka lazima yachukue muundo wa silabi wazi. Maneno mageni kutoka Kiingereza yanayoingia katika Kitharaka ndiyo hudhahirisha uchopekaji wa irabu mwishoni mwa neno. Mantiki ya hali hii ni kwamba, maneno mengi ya Kiingereza huwa yenye silabi funge. Mfano wa maneno kama haya umetolewa hapa chini.

Kiingereza	Kitharaka	Othografia
[net]	→	[neti] net
e→ε		
ø→i/#...		
 [mædʒɪk]	→	 [manJeki] magic
æ→a		
dʒ→nʃ		
i→e		
ø→i/#...		

Maneno mengi katika Kiingereza huwa na silabi funge, hususan silabi ya mwisho katika neno. Kutokana na hali hii, maneno mageni kutoka Kiingereza

yanapoasilishwa katika Kitharaka, hulazimika kuchopekwa irabu mwishoni mwa neno ili kuifanya silabi ya mwisho kuwa wazi. Kwa jumla, sheria ya kimsingi inayotawala uchopekaji wa sauti katika mazingira yote ya neno lililoasilishwa katika Kitharaka ni hii.

- a)  $\emptyset \rightarrow I(K)/\dots \# au I/\# \dots$
- b)  $\emptyset \rightarrow I/\#K\dots K\#$

### Kuimarika kwa Fonimu

Vitamkwa hutofautiana kulingana na nguvu zinazotumika kuvitamkia. Akizungumzia suala hili, Mgullu (1999), anasema kwamba imebainika kuwa sauti hafifu hutumia nguvu nyingi kutamkika. Kwa hiyo, sauti hizo zinakuwa imara. Aidha, sauti ghuna hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo; kwa hivyo; ni dhaifu. Katika hali hii, kuimarika kwa fonimu hutokea wakati ambapo kitamkwa mahususi hubadilika kutoka kuwa ghuna na kuwa kisichoghunga. Katika hali ya awali, yaani kitamkwa kuwa na ughuna, kuna kudhoofika kwake, ilhali katika hali ya pili, kitamkwa kuwa na uhafifu huwa ni kuimarika kwake. Mchakato wa kuimarika kwa fonimu hujitokeza katika maneno mageni yaliyoasilishwa katika Kitharaka kwa namna tofauti kama ifuatavyo:

Kiswahili		Kitharaka
[ndɛgɛ]	→	[ndɛkɛ]
g→k		
[mwalimu]	→	[mwarimo]
l→r		
Kiingereza		Kitharaka
[Səʊlə]	→	[cɔ:ra]
l→r		

Maneno mageni yenye sauti /g/ yakiasilishwa, sauti /g/ hugeuka na kuwa /k/. Katika hali hii, sauti /g/ ni ghuna ilhali sauti /k/ ni hafifu. Hivi ni kusema kwamba, sauti /g/ ni dhaifu kutokana na sifa yake ya kutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo. Kwa upande mwingine, sauti /k/ ni imara. Hii ni kwa sababu, msemaji hutumia nguvu nyingi kuitamka. Katika hali hii tunaweza kusema kwamba sauti /g/ inaimarika inapobadilika na kuwa sauti /k/. Vivyo hivyo, hali ya kuimarika kwa fonimu inadhihirika kwenye maneno mageni yaliyoendelezwa kwa kutumia sauti /l/, ambayo inabadilika na kuwa /r/ katika maneno yaliyoasilishwa. Katika mchakato huu, kitambaza /l/ hutumia nguvu kidogo ikilinganishwa na kimadende /r/. Hii ni kwa sababu katika ngazi za sauti, kitambaza kiko chini kuliko kimadende kwa mujibu wa nguvu inayotumika kukitamka (Mgullu, 1999; Obuchi na Mukhwana 2015). Kutokana na hali hii, kitambaza /l/ ambacho ni dhaifu kinaimarika na kuwa kimadende /r/ ambacho hutamkwa kwa kutumia nguvu nyingi.

---

Kuchukuliwa kwa nafasi ya kitambaza /l/ na kimadende /r/ katika Kitharaka hutokana na hali ya kukosekana kitambaza /l/ katika fonolojia wa Kitharaka. Ukosefu wa sauti /l/ katika Kitharaka hupelekea msemaji kutumia sauti /r/ kwa mantiki kwamba sauti hizo ndizo hukaribiana kimatamshi.

### **Kudhoofika kwa Fonimu**

Mchakato huu unapelekea fonimu inayotumia nguvu nyingi, yaani hafifu kubadilika na kuwa ghuna, sauti ambayo hutumia nguvu kidogo. Katika Kitharaka, baadhi ya fonimu hudhoofika zinapokuwa katika maneno mageni yaliyoasilishwa. Hapa chini kuna mifano ya fonimu zinazodhoofika wakati maneno yanaasilishwa katika Kitharaka.

<b>Kiswahili</b>	→	<b>Kitharaka</b>
[kiʃikɔ]		[gecikɔ]
k→g		
[pikipiki]	→	[bikibiki]
p→b		
<b>Kiingereza</b>	→	<b>Kitharaka</b>
[peli:s]		[borici]
p→b		

Maneno mageni kutoka Kiswahili yaliyo na sauti /k/ yanapoasilishwa, sauti hiyo hubadilika na kuwa sauti dhaifu /g/. Sauti /k/ ni kitamkwa kilicho hafifu; kwa hivyo, nguvu inayotumika kukitamkia ni nyingi; hali inayopelekea kuwa imara. Katika hali hii, kitamkwa /k/ huwa kimebadilika na kuwa kitamkwa /g/ katika neno lenye maana ileile katika Kitharaka. Hivyo, kitamkwa /k/ kimeimarika na hali hii hutokeea kwenye mifano ya maneno mageni kutoka Kiingereza na vilevile Kiswahili wakati maneno yenye sauti /p/, ambayo ni imara, hubadilika na kuwa sauti dhaifu /b/.

### **Ukaakaishaji**

Mchakato huu unapotokea, fonimu zisizo za kaakaa hubadilika na kuwa za kaakaa. Kitharaka kina fonimu kumi na moja za kaakaa /c, ſ, nc, nʃ, jn, k, g, ŋk, ŋg, ŋ, j/. Katika Kitharaka kikwamizo /c/ ndiyo sauti ya kaakaa ambayo inahusishwa na ukakaishaji kwa wingi. Tazama mifano ifuatayo:

<b>Kiingereza</b>	→	<b>Kitharaka</b>
[θɜ:rməs]		[θamɔci]
s→c		
[ʃɪln̩]	→	[ciringi]
ʃ→c		

Katika mifano ya maneno mageni yaliyochunguzwa, mchakato wa ukakaishaji unahusisha sauti /s/ na /ʃ/ kubadilika na kuwa sauti /c/. Katika hali hii, sauti /s/ na /ʃ/ ambazo ni za ufizi zinabadilisha sehemu asili ya kutamkiwa na kuanza kutamkiwa kwenye kaakaa gumu. Kwa jinsi hii, sauti /s/ na /ʃ/ zikawa zinaathiriwa na mchakato wa ukakaishaji na kuwa sauti /c/ ambayo ni ya kaakaa ngumu. Aidha, kuna hali ya ukakaishaji katika maneno mageni kutoka Kiswahili wakati yanapoasilishwa katika Kitharaka.

Kiswahili		Kitharaka
[mʃahara]	→	[mocara]
f → c		
[sadaka]	→	[candaka]
s → c		

Maneno ya Kiswahili yanayoingia katika Kitharaka huathiriwa na ukakaishaji kwa namna sawa na ile ya maneno mageni kutoka Kiingereza. Katika hali hii sauti /s/ na /ʃ/ hubadilika na kuwa /c/ ya kaakaa gumu.

### Ung'ong'oishaji

Utaratibu wa kung'ong'oisha fonimu unahusisha sauti isiyo na sifa ya ung'ong'o kutamkwa ikiwa ama na unazali hafffu au kuwa nazali kamili. Katika Kitharaka, fonimu za ving'ong'o /m/ na /n/ ndizo huhushishwa katika ung'ong'oishaji.

Kiingereza		Kitharaka
[bæg]	→	[mbagi]
b → mb		
[dʒæg]	→	[nJagi]
dʒ → nJ		
Kiswahili		Kitharaka
[dawa]	→	[ndawa]
d → nd		

Maneno mageni yaliyo na konsonanti za vidasuo /b/, /d/ na kikwamizwa /ʃ/ ndio mara nyingi huathiriwa na ung'ong'oishaji. Katika hali hii, sauti hizi hupata ung'ong'o hafffu na kuwa vikocha vya ving'ong'o kwa jinsi hii:

/b/	→	/mb/
/d/	→	/nd/
/ʃ/(dʒ)	→	/nʃ/

Pia, ung'ong'oishaji huweza kufanikishwa na usilimisho, hali inayotokea wakati sauti moja inaathiriwa na nyingine kwa sababu ya kukaribiana nayo. Athari

inayotokana na usilimisho inaweza kuwa ung'ong'oishaji. Kwa mifano, katika neno [mbagi], sauti /n/, (ambayo ni ya umbo la ndani la neno hili) inapopakana na sauti /b/, hali ya usilimisho mbele hutokea. Usilimisho huu hupelekea sauti /b/ kuwa na ung'ong'o kiasi kwamba itabadilika na kuwa kikocha cha nazali /mb/. Kimsingi, sauti hii inapaswa kuwa /nb/, lakini muundo wa Kitharaka hauruhusu mpangilio wa aina hii wa sauti.

### **Usilimisho**

Usilimisho hueleza jumla ya athari za sauti moja kwa nyingine zinazoleta ukuruba wa kimuundo. Sauti husilimisha nyenzake kwenye mojawapo ya hali mbili: Pahala pa kutamkia na jinsi ya kutamka. Sauti husilimisha nyingine kwa kuifanya itamkiwe katika mahali tofauti na pale inapotamkiwa katika hali ya kawaida. Pia, sauti inaweza kuwa na athari dhidi ya jinsi ya kutamka sauti jirani. Usilimisho unabainika kwa jinsi mbili: Kwa kutegemea mazingira ya sauti inayosilimishwa: Usilimisho mbele au usilimisho nyuma. Usilimisho nyuma wa pahala pa kutamkia hutokea kwa wingi pale ambapo sauti ya nazali inaambatana na vidasuo. Katika mwambatano kama huu, sauti ya nazali /n/ husilimishwa na kipasuo /b/, ili itamkiwe kwenye sehemu ya midomo. Kuhusiana na maelezo haya, inatubidi tuangalie mifano ifuatayo:

Neno	Hali ghafi (Kitharaka)	Hali kamilifu (Kitharaka)
box	n+bogici	mbogici
bible	n+baibû	mbaibû

Kutokana na mifano hii, nomino zilizotolewa zinaonekana kuwa katika kundi la ngeli ya *N~N*. Hata hivyo, sauti /n/ haidhahiriki kutokana na athari za usilimisho nyuma unaoletwa na sauti /b/. Katika hali hii, sauti /n/ ambayo ni king'ong'o cha ufizi hubadilika na kuwa king'ong'o cha midomo /mb/.

### **Usilabishwaji**

Uasilishaji wa maneno mageni hauwezi kujitenga na mabadiliko ya muundo wa silabi yanayojitokeza pindi maneno haya yanapoingia kwenye lugha pokezi. Hii ni kwa sababu silabi ni kipashio cha fonolojia arudhi ambacho pia hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Akizungumzia suala hili, Hyman (1975), anasema kuwa, usilabishwaji unahuksu kanuni zote zinazoelekeza uundaji wa silabi kwa kuzingatia utaratibu wa kifonotatiki, uwekaji wa mipaka ya silabi. Hivyo basi uainishaji wa maumbo na miundo mbalimbali ya silabi.

Usilabishwaji wa maneno mageni ni mchakato wa kifonolojia ambao hujiri kutokana na athari zinazoletwala na michakato mingine (Buliba, 2001). Usilabishwaji, basi, ni zao la michakato mingine ya kifonolojia kama vile uchopekaji wa sauti. Kutokana na hali hii, neno la Kiingereza #spring# [sprɪŋ] lenye silabi moja ya muundo wa \$KKIK\$ linapoasilishwa katika Kitharaka, muundo na idadi ya silabi hubadilika. Uasilishaji huu hupelekea neno hili kutamkwa:[cibirinj]. Mabadiliko haya ya muundo wa silabi baada ya kuasilishwa

kwa neno husika hupelekea idadi ya silabi kuongezeka na kuwa nne za muundo wa KI: \$ci\$bi\$ri\$\\$nji\$. Katika neno hili, michakato kadhaa imehusika katika kapatikana kwa mabadiliko haya ya idadi, muundo na maumbo ya silabi za neno husika. Kwanza, kumetokea mchakato wa ukaakaishaji wa sauti /s/ ambayo ni ya ufizi. Sauti hii hubadilika na kuwa /c/ ambayo ni sauti ya kaakaa gumu. Pili, kumetokea hali ya kudhoofika kwa fonimu ambapo Sauti inayotumia nguvu nyingi ( /p/) hubadilika na kuwa sauti hafifu (/b/). Tatu, mchakato wa uchopekaji hutokewa wakati ambapo sauti ya irabu /i/ imechopekwa baina ya konsonanti /c/ na /b/. Pia, irabu /i/ imechopekwa baina ya /b/ na /r/, na mwishoni mwa neno. Uchopekaji wa irabu baina ya konsonanti hutokana na haja ya kuvunja mfuatano wa konsonanti ambaa unakubalika katika Kitharaka; mtindo huu haupendelevi na lugha ya Kiingereza. Hatua ya kuvunja mfuatano wa konsonanti inapelekea kupatikana kwa silabi ya muundo wa KI. Huu ndio muundo ambaa unakubalika na kupendelewa katika mfumo wa fonolojia ya Kitharaka. Katika uchanganuzi wa neno [sprɪŋ] ambalo ni la Kiingereza, tunapata maumbo ya silabi hii yenye muundo wa \$KKKIK\$.

Licha ya uchopekaji kubadilisha idadi ya silabi, pia, umepelekea kubadilisha silabi fungo kuwa wazi. Irabu /i/ inayochopekwa mwishoni mwa neno[sprɪŋ] imesababisha kupatikana kwa silabi wazi ya \$\\$nji\$. Usilabishwaji wa maneno mageni kutokana na maneno ya Kiingereza pia huletwa na hali ya kuweko kwa aina tatu tofauti za irabu katika Kiingereza; yaani irabu fupi, irabu ndefu na irabu unganifu. Lugha ya Kitharaka haina irabu ndefu ama irabu unganifu. Hivyo, tunapata kwamba silabi nzito inayoundwa kwa kilele cha irabu ndefu haipo katika Kitharaka.

Kwa mujibu wa Buliba (2001), neno la Kiingereza lililo na silabi nzito linapoingia katika Kiswahili, uzito hudondoshwa pamoja na ule urefu wa irabu. Katika mwelekeo sawa na huu, silabi nzito inayosababishwa na irabu ndefu, inapoasilishwa katika mfumo wa fonolojia ya Kitharaka, uzito hudondoshwa na kuwa silabi nyepesi iliyo wazi. Kwa mfano, neno #nursery# [nɜ:səri] lina silabi \$nɜ:\$ ambayo ni nzito kutokana na kuwepo kwa irabu ndefu [ɜ:]. Hata hivyo, katika uasilishaji wake katika Kitharaka, irabu /ɜ:/ inabadilika na kuwa /a/ ambayo ni irabu fupi ama ya kawaida. Katika hali hii, mabadiliko yanayotokea kwenye irabu, pia husababisha badiliko la silabi; yaani silabi nzito \$nɜ:\$ inabadilika na kuwa silabi nyepesi \$na\$. Akizungumzia kauli hii, Mbugua (1990) anasema kwamba silabi nzito huundwa kwa kina cha irabu ndefu, mseto wa irabu ndefu na konsonanti moja au mseto wa irabu fupi na konsonanti mbili au zaidi. Kwa upande mwingine, silabi nyepesi huundwa kwa kina cha irabu fupi, irabu unganifu au mseto wa konsonanti na irabu fupi. Vilevile, mchakato wa usilabishwaji hujitokeza kwenye maneno mageni kutoka Kiswahili yanayoingia na kuasilishwa katika Kitharaka.

Lugha zote mbili hupendelea muundo wa silabi wa KI, japo zinatofautiana kwa kiasi fulani ambapo maneno mageni kutoka Kiswahili yaliyo na silabi fungo hubadilika na kuwa silabi wazi kwa kuchopekwa irabu baina ya konsonanti. Silabi

funge katika Kiswahili huundwa kwa sauti za king'ong'o /m/ na /n/. Mifano ya maneno yenye silabi funge zinazoundwa na ving'ong'o pekee ni pamoja na:

<b>Kiswahili</b>	<b>Kitharaka</b>
[m\$ke\$be]	[mo\$ke\$be]
[m\$ka\$te]	[mo\$ga\$te]

Katika mifano ya hapo juu, silabi ya mwanzo wa maneno katika ngeli ya kimofolojia ya **M-MI** katika Kiswahili, hali ya umoja huwa ni fungo na yenye muundo wa konsonanti (K) pekee. Silabi ya aina hii ikilinganishwa na silabi ya neno lilo hilo linapoasilishwa na kuingizwa katika Kitharaka huwa tofauti kwa vile umbo na muundo wake hubadilika. Silabi hii hugeuka na kuwa wazi. Mfano wa silabi \$m\$ katika neno 'mkebe' \$m\$ke\$be\$ na 'mkate'\$m\$ka\$te\$ pamoja na mabadiliko yake ni ithibati inayoonyesha jinsi silabi funge inavyopitia mchakato wa usilabishwaji ili kuafiki muundo wa silabi katika lugha ya Kitharaka.

Aidha, kuna maneno mageni kutoka Kiswahili ambayo yanadhihirisha uchopekaji wa silabi nzima katika neno. Katika hali hii, silabi katika neno huongezeka wakati neno husika huasilishwa. Mfano wa maneno kama hayo ni:

<b>Kiswahili</b>	<b>Idadi ya Silabi</b>	<b>Kitharaka</b>	<b>Idadi ya Silabi</b>
[ču\$pa]	2	[mo\$co\$ba]	3
[gɔ\$dɔ\$rɔ]	3	[mo\$kɔ\$ndɔ\$rɔ]	4
[i\$nJi\$li]	3	[e\$gwa\$nJe\$ri\$ɔ]	5

Sababu inayopelekea kuongezeka kwa idadi ya silabi ya maneno mageni yanapoasilishwa ni kuwa silabi inayoongezewa huwa ni kiambishi awali cha ngeli. Hapa, uasilishaji wa neno geni pia huopelekea neno husika katika ngeli ya nomino inayofaa kulingana na Kitharaka. Kwa hiyo, mabadiliko haya huwa ni ya kimofofonolojia. Kwa mfano, maneno [ču\$pa] na[gɔ\$dɔ\$rɔ] yanapatikana katika ngeli ya *N~N* katika Kiswahili. Hata hivyo, maneno yayo hayo yakiasilishwa katika Kitharaka, huingia katika ngeli ya *M~MI*. Mabadiliko haya yanatokana na mchakato wa usilabishaji. Mchakato huu huyafanya kuwa [mo\$co\$ba] na [mo\$kɔ\$ndɔ\$rɔ] mtawalia.

### **Uwiano wa Irabu**

Uwiano wa irabu ni mchakato unaopatikana katika maneno mengi ya Kibantu. Irabu ya mzizi wa kitenzi huathiri irabu inayotokea katika mnyambuliko wa kitenzi hicho. Uwiano wa irabu, basi, ni utaratibu wa irabu fulani kukubali kuandamana katika mazingira maalumu (Mgullu, 1999, Obuchi na Mukhwana 2015). Uwiano wa irabu hufuata shuruti fulani. Kwa mfano, katika Kiswahili, iwapo mzizi wa kitenzi katika hali ya mnyambuliko wa kauli ya kutendea una irabu /a/, /i/ au /u/ kiambishi tamati cha mnyambuliko huwa {i}. Ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu /ɔ/ au /ɛ/ kiambishi tamati cha mnyambuliko sharti kiwe{ɛ}. Kuna vitenzi vilivyoasilishwa kutokana na

Kiswahili ambavyo hudhihirisha uwiano wa irabu hata vikiwa katika hali kamili ya uasilishaji wake katika Kitharaka. Turejelee mifano hapa chini:

<b>Kitenzi</b>	<b>Mzizi</b>	<b>Kutendea</b>
andika	{andik}	andik- i-a
cheza	{chez}	chez- e-a
<b>Kitharaka</b>		
andika( andika)	{andik}	andik- ir-a
cetha ( cheza)	{ceth}	ceth- er-a

Katika mifano ya maneno mageni haya, dhana ya uwiano wa irabu inahamishiwa katika lugha pokezi. Hata hivyo, kuna maneno asilia katika Kitharaka ambayo hudhihirisha mfanyiko wa uwiano wa irabu. Vitenzi vifuatavyo vimenyambuliwa katika kauli ya kutendea katika Kitharaka.

<b>Kitenzi</b>	<b>Mzizi</b>	<b>Kutendea</b>	<b>Maana</b>
ina ( imba)	{in}	in- ir-a	imbia
theka (cheka)	{thek}	thek-er-a	chekelea
roar (rina)	{ror}	ror-er-a	rinia

Katika mifano iliyopo juu, inabainika kwamba irabu inayounda mzizi hushurutisha kiambishi cha mnyambuliko kuwa na irabu inayotokea kwa utaratibu maalumu. Utaratibu huu unawiana katika maneno yote yaliyoundwa na mzizi wenyewe irabu ya aina moja. Kwa mfano, maneno yaliyotokana na mzizi wenyewe irabu /i/, /a/ au /u/ kiambishi cha mnyambuliko huwa na irabu /i/. Vivyo hivyo, maneno yaliyotokana na mzizi wenyewe irabu /ɛ/ au /ɔ/ kiambishi cha mnyambuliko huwa na irabu /ɛ/.

### Hitimisho

Makala haya yamejadili michakato ya kifonolojia na uasilishaji wa maneno ya kigeni katika Kitharaka. Michakato ya kifonolojia ni muhimu katika kufanikisha uasilishaji wa maneno ya kigeni katika lugha pokezi yoyote ile. Michakato hii ndiyo husababisha ama mageuko ya fonimu, mwongezeko wa fonimu katika neno au mpishano wa sauti katika neno lililoasilishwa. Hali hizi zote huchangia sana kwa neno geni kuafikiana na mfumo wa kifonolojia wa lugha husika. Ukopaji na uasilishaji wa maneno katika lugha ni hatua muhimu katika lugha yoyote ile kwa sababu huchangia kukua na kupanuka kwa lugha ili iweze kukidhi haja ya mawasiliano. Kipindi hiki cha utandawazi, lugha nyingi za Kiafrika zinawania kuhodhi msamiati wa kigeni ili kufanikisha mawasiliano na uelewa wa jinsi uasilishaji unaweza kuelekezwa ili kukuza lugha ni muhimu kwa wataalamu wa lugha ili kusiwe na vurugu katika lugha zinazokua. Ifahamike kwamba lugha za ulimwengu hukopa msamiati ama huathiriwa na lugha zingine za ulimwengu. Kutokana na hali hii, inapendekezwa kwamba kuna haja ya kupanua suala la

uasilishaji katika lugha nyingi za Kiafrika kadri iwezekanavyo ili kupanua uelewa wa mifanyiko ya uasilishaji na jinsi ya kutumia michakato ya uasilishaji kustawisha lugha hizo. Mwelekeo huu utapanua fonolojia ya lugha za Kiafrika ambazo hazijatafitiwa kwa wingi katika kiwango cha fonolojia.

**Marejleo**

- Anderson, J. M. (1973). *Structural Aspects of Language Change*. New York: Longman.
- Appel, R. and Muysken, P. (1987). *Language Contact and Bilingualism*. London: Edward Arnold.
- Buliba, F. O. (2001). Uswahilishaji Kifonolojia wa Maneno yenye Asili ya Kiingereza katika Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Njoro: Chuo Kikuu cha Egerton.
- Crystal, D. (1987). *Cambridge Encyclopedia of Languages*. Cambridge: CUP.
- Crystal, D. (1987). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics* (2<sup>nd</sup>Edition). Oxford: Blackwell Ltd.
- Gillian, S. and Suzanne, L.(1972). “On the Acquisition of Native Speakers by a Language” in *Round Table on Languages and Linguistics* vol 6 pp 73-84 Georgetown: Georgetown University.
- Hearth, J. (1994). “Borrowing” In *The Encyclopedia of Languages and Linguistics*. Vol. 1(pp292-295) Oxford: Pergamon Press.
- Hudson, K. P.(1980). *Phonological Adaptation of Loanwords*. Oxford: Black Well.
- Hyman, L. M. (1975). *Phonology: Theory and Analysis*. Holt Rinehart, Winston: San Fransisco.
- Hyman, L. M. (1970a). “The role of Borrowing in the Justification of Phonological Grammars” In *Studies in African Linguistics* Vol. 1(pp 187-198).
- Kadurenge, B. M. (2000). Mabadiliko ya Kifonolojia katika Msamiati unaosharabiwa kutoka Kiswahili hadi Kimaragoli. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi.
- Katamba, F. (1989). *Learning About Language: An Introduction to Phonology*. London: Longman Group (UK) Limited.
- Mbugua, A. N. (1990). *A Phonological Reality of the Syllable*. Unpublished M.A Thesis: Kenyatta University.
- Mgullu, R. S. (1999). Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili. Nairobi: Longhorn Publishers.

- Mosha, M. (1970). "Loanwords in Luganda: A Search for Guides in the Adaptation of African Languages to Modern Conditions" In W. H. Whiteley (Ed.) *Language Use and Social Change: Problems of Multilingualism with Special Reference to Eastern Africa.*(pp231-256). London: Oxford University Press.
- Mukuthuria, M. (2008) "Uchunguzi wa Athari Kama Nyenzo ya Kufunza Lugha." Katika N. O. Ogechi, N. I. Shitemi na K. I. Simala (whr). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* (uk 375-386). Eldoret: Moi University Press.
- Mukuthuria, M. (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Tigania Kenya.* Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Njoro: Chuo Kikuu cha Egerton.
- Mwihaki, A. N. (1998). Loanwords and Nativization. A Generative View of Phonological Adaptation of Gikuyu Loanwords. Unpublished Ph.D Dissertation. Kenyatta University.
- Mwita, L. C. (2009). "The Adaptation of Swahili Loanwords from Arabic: A Constraint-Based Analysis" In *The Journal of Pan African Studies.* Vol 2. No.8. pp 70-89.
- Zawawi, S. (1974). Loanwords and their Effects on Classification of Swahili Nominals. Ph.D Dissertation. Colombia University.

